BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA (OR), TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

---

**Mheshimiwa Spika:** Kila sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Baraza la Kumi kwa dhamira ya kujadili Bajeti kuu ya Serikali na Taasisi zake katika chombo hiki kitukufu nchini. Kwani hii ni rehma yake Muumba kwa kutupa pumzi na afya njema ambayo wenzetu wengine amewanyima fursa hii na wakati huu wameshindwa kutimiza malengo yao.

**Mheshimiwa Spika:** Kipekee, nitumie fursa hii kutoa shukrani na pongezi za pekee kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi imara wa Rais wetu mpendwa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika uongozi wake na kuhakikisha maendeleo ya Tawala za Mikoa, Idara maalum pamoja na

Serikali zetu za Mitaa nchini yanaimarika siku hadi siku kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika:** Pia, napenda kutumia fursa hii adhimu kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele yako, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na ***Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2024/2025*** kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2020* zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika:** Vilevile, niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati viongozi wa Ofisi hii wakiongozwa na Waziri wao hodari na mchapakazi sana Mheshimiwa Masoud Ali Mohammed, Katibu Mkuu Ndugu Issa Mahfoudh Haji na Afisa Mdhamini Pemba Ndugu Thabit Othman Abdalla. Aidha, niwapongeze Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya, Makamanda wa Vikosi vya Idara Maalum za SMZ na watendaji wote wa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha katika Kamati yetu na kuchangia kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika:** Pamoja na hayo, Kamati yetu inatoa

pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Suzan Peter Kunambi kwa kuteuliwa na Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT) kwa hakika Mhe. Suzan ni mchapakazi hodari, mwaminifu na mwenye weledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yake. Kamati inamtakia kila la heri katika majukumu yake mapya, tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amfanyie wepesi kwa kila hatua ili aweze kutimiza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa umuhimu wake, naomba kutumia nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutumia na kutekeleza vyema ushauri na miongozo ya Kamati pamoja na kusimamia kwa ukamilifu mipango ya utekelezaji wa programu zilizoainishwa katika Bajeti ya mwaka *2023/2024*, jambo hili limewawezesha kujenga ari ya kuwasilisha mbele ya Kamati yetu, pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio mapya ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha *2024/2025* ili yapate baraka za Wajumbe wako na kwa muktadha huo, tunaliomba Baraza lako tukufu liridhie na liipitishe Bajeti hii kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa namna ya pekee, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya Wajumbe wa

Kamati yangu wakati tulipoipitia bajeti hii, kwa kuonesha umahiri na mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii.

Naomba sasa niwatambue Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | M/Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Haji Shaaban Wazir | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika:** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imetumia vyema nafasi yake katika kupitia, kuchambua na kujiridhisha na programu zote zilizopangwa kufanyiwa kazi kupitia Mafungu ya Bajeti ya Ofisi hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2020*.

**Mheshimiwa Spika:** Ni imani ya Kamati hii kwamba kupatikana kwa fedha zilizokadiriwa kutumika katika Ofisi hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa malengo yake katika kipindi husika ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi mbali mbali ya kimaendeleo inayotekelezwa kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

## PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU (FUNGU D 01)

**Mheshimiwa Spika:** Kupitia Programu Kuu ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;** Kamati imebaini kuwepo kwa kiwango kidogo cha mapato kilichokusanywa kupitia vyanzo vya mapato katika Halmashauri za Mabaraza ya Miji na Mikoa ambapo imeelezwa kuwa uhaba wa vyanzo vya mapato na vifaa vya kisasa ni njia moja wapo iliyopelekea kupungua kwa mapato hayo. Katika suala hili, Kamati kupitia mafungu ya Mikoa imegundua kwamba baadhi ya Mikoa ilipangiwa kukusanya kiwango kikubwa cha mapato bila kuangalia uwezo wa vyanzo vya mkoa husika pamoja na nguvu ndogo ya ukusanyaji wa mapato kwa Halmashauri na Mabaraza ya Miji na Manispaa. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Taasisi hizi kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya ulipaji wa tozo na ada ili kuongeza kasi ya mapato kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika:** Katika programu ndogo ya **SD010102** ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa** yenye lengo kuu la kuongeza ufanisi wa kiutendaji na upatikanaji wa huduma za jamii, Kamati yangu inapata mashaka kwamba lengo la programu hii halitofikiwa kutokana na changamoto za vifaa ambazo zinazikabili Halmashauri zetu, kwa mfano katika Manispaa ya Chake – Chake, Manispaa ya Kaskazini A, Baraza la Mji Wete, Kaskazini B Unguja pamoja na Baraza la Mji Kati kwa pamoja wanakabiliwa na changamoto ya magari ya kukusanyia taka, magari ya kuzolea taka (scavetta). Ukosefu huu unazifanya taasisi hizi kushindwa kufikia malengo yake katika jukumu la usafi na hivyo kuonekana na nguvu ndogo ya kuweka miji safi na kuchangia miji yetu kutokuwa na haiba nzuri siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa namna hiyo, Kamati inaomba Serikali kupitia Bajeti hii kuanda mpango maalumu utakaoziwezesha Halmashauri zetu kupatiwa vifaa vya kisasa vyenye uwezo wa kuleta mageuzi katika upande wa mapato na usafi wa miji. Hata hivyo, Kamati inazishauri Serikali za Mikoa kusimamia changamoto hizo kwa kuendelea kuzitafutia ufumbuzi na kuweka mazingira safi na yenye haiba kwa wananchi na wageni. Kadhalika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kusaidia upatikanaji wa magari na vifaa vyengine vya ukusanyaji taka katika Baraza la Manispaa ya Magharibi "A".

**Mheshimiwa Spika:** Kamati yangu pia, inaitaka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia programu ndogo ya **SD010101** ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa** kuhakikisha wamesimamia vyema majukumu ya ulinzi na usalama kwa kulinda amani iliyopo na kuacha kuwafumbia macho vijana wanaoharibu amani na usalama wa raia. Kwa mantiki hiyo, Kamati inazitaka kamati za ulinzi na usalama kwa kila Mkoa kuhakikisha wamepambana vya kutosha katika kupiga vita makundi maovu ya vijana ambayo yanahatarisha usalama wa wananchi na mali zao. Sambamba na hayo, Kamati inashauri Serikali za Wilaya kupitia programu hii kutoa elimu kwa wananchi juu ya mapambano dhidi ya wizi wa mazao na mifugo mijini na vijijini pamoja na kuchukua hatua kali kwa watu wenye tekeleza tabia hizo.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati yangu inaunga mkono juhudi za ujenzi wa masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini kwa hatua iliyofikiwa tukiamini kwamba kukamilika kwa masoko haya makubwa na ya kisasa kutachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa ajira kwa vijajana wetu. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuzidisha kasi ya usimamizi wa miradi hii ili iweze kukamilika kwa wakati na kuondosha usumbufu unaopatikana sasa kutokana na kutokuwepo kwa masoko ya uhakika katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa upande wa miundombbinu ya masoko kamati imeridhika na namna masoko haya yalivyosanifiwa kujengwa na yatakapokamilika yatakua masoko ya kupigiwa mfano kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki. Sambamba na hayo, Kamati inashauri kwa upande wa soko la Chuini kutengenezwa mtaro ambao utasaidia kuondoa maji ya mvua kutoka sokoni na kuelekezwa baharini kwa lengo la kuondosha maji yanayotuwama katika eneo la soko.

Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutumia vyema fedha za nyongeza za Bajeti (Supplementary Budget) ambazo ziliombwa kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa masoko. Vile vile, Kamati inaishauri Serikali miradi mikubwa kama hii kuendelea kuwaamini na kuwapa vijana wetu wa Idara Maalum za SMZ kutokana na kujenga kwa kufuata wakati na kupungua kwa gharama za ujenzi.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa upande wa masoko ya wajasiriamali ambayo yamekamilika na kutumika kwa muda mrefu sasa, Kamati inasikitika na kuona mwamko mdogo wa wananchi katika matumizi ya masoko haya na hivyo kufanya kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kwa hivyo, Kamati inaishauri jamii kuyatumia kikamilifu masoko ya wajasiriamali ambayo

yamejengwa takribani kila Wilaya kwa upande wa Unguja na Pemba ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira.

**Mheshimiwa Spika:** Katika programu ndogo ya **SC010403** ya **Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba** yenye lengo la kuweka mazingira mazuri kwa Ofisi na Wafanyakazi Pemba utekelezaji wake utakua na ugumu kutokana na changamomto ya jengo la Ofisi na ukosefu wa vyombo vya usafiri. Kamati inaishauri Serikali kufanya utaratibu wa kujenga upya jengo la Ofisi hii ili kuwajengea watendaji mazingira bora ya kazi.

**Mheshimiwa Spika:** Kwenye Programu ndogo ya **SD010404** ya **Kuratibu Jumuiya zisizo za Kiserikali;** Kamati imeridhika na namna taasisi hii inavyotekeleza majkumu yake na kuhakikisha kwamba jumuiya zote zinatimiza wajibu wake kwa mujibu wa taratibu za nchi. Kamati inazipongeza Jumuiya hizi kwa namna zinavyosaidia jamii katika masuala mbali mbali ikiwemo kujenga uelewa juu ya athari ya matendo ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, kutoa misaada ya kijamii na kusaidia katika ujenzi wa miundombinu. Hata hivyo, tunaishauri Serikali kuziwezesha jumuiya hizi kwa kuwapatia mafunzo ya kitaalamu juu ya uandishi bora wa miradi wanayohitaji kuitekeleza.

## PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D 02 – D 06):

**Mheshimiwa Spika:** Kwa upande wa programu za Idara Maalum za SMZ ambazo programu yake kuu ya Uratibu na Usimamizi wa Idara Maalum inatekelezwa kupitia **fungu D01** la Ofisi Kuu kwa lengo la kuweka uwiano wa Idara zote za SMZ katika masuala ya kiutawala. Kamati imeridhika na kazi nzuri za wapiganaji wetu wa vikosi vya SMZ kwa kushirikiana na vikosi vya SMT kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kuhakikisha tunu ya amani na utulivu tuliyonayo imedumu katika nchi yetu, tumuombe Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na kuwapa uzalendo askari wetu wa kuitumikia vyema nchi yao.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati kupitia programu ndogo ya **SD0100201** ya **Usimamizi wa Utumishi na Uratibu;** Kamati inaishauri Tume ya Utumishi ya Idara Maalum kuhakikisha programu hii imekamilika na kufikiwa malengo yake kwa kuboresha mazingira ya kazi za askari wetu pamoja na kupatiwa mafunzo muda mrefu na muda mfupi ili kusaidia vikosi vyetu kuwa na uelewa juu ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo kwasasa dunia imebadilika

katika utendaji wake.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati inazidi kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za kuviimarisha vikosi vya SMZ na kuimarisha maslahi ya wapiganaji wote wa Idara maalumu. Aidha, pongezi za pekee ziende kwa Wakuu wa Vikosi vyote vya SMZ kwa juhudi zao za kusimamia vyema majukumu waliyopewa pamoja na kuibua miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika idara zao.

**Mheshimiwa Spika:** kamati imeridhika na utendaji wa JKU sambamba na mipango yake ya uzalishaji mali na kutoa huduma za afya na ulinzi kwa viongozi wetu. Hivyo, kupitia **Fungu D02 JKU;** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha miundombinu ya kilimo katika kambi mbali mbali za JKU kwa lengo kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao ya chakula na mifugo ili kupunguza uhitaji wake kutoka nje ya visiwa vyetu. Hata hivyo, Kamati yangu hairidhiki na matumizi makubwa ya eneo na shamba la Bambi ambalo linatumiwa na Muwekezaji wa Misri ambaye hana manufaa yoyote kwa JKU badala yake anawasababishia gharama za uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika:** Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kupitia programu kuu ya ***Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo,*** Kamati imeridhika kwa namna programu hii inavyotekelezwa na kupata

matukio mazuri ambayo ndio lengo la Serikali kwa upande wa KMKM katika kusaidia kulinda na kukuza uchumi wa nchi. Hata hivyo, kamati hairidhiki na hali ya upatikanaji wa mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa operesheni za baharini kutokana na uingizwaji mdogo wa fedha za matumizi mengineyo (OC). Aidha, kamati inaishuri Serikali kuweka fungu maalumu la mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa operesheni hizo ili kutimiza lengo la udhibiti wa magendo na uhujumu uchumi unaofanywa kupitia njia ya bahari.

Sambamba na hayo, Kamati yetu inaipongeza Wizara kwa kuleta mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya KMKM Namba 1 ya Mwaka 2003 ambapo marekebisho yatafanywa kwa lengo la kukiwezesha kikosi kufanya shughuli za kiuchumi, biashara na uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika:** Kwa upande wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi **Fungu D05** Kamati inasisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokozi katika Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar ili kuwa bora na kuendelea kupata hadhi kimataifa. Kamati pia, inaishauri Serikali isimamie kufanyika mapitio ya Sheria nambari *7* ya mwaka *1999* ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kwa lengo la kukuza ufanisi wa kazi zake katika viwanja vya ndege na makaazi ya watu. Aidha, Kamati inashauri kikosi hiki cha Zimamoto na Uokozi kupatiwa fedha

za ziada kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ambayo yanatumika kwenye shughuli zao za uokozi katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika:** Katika kujenga mazingira bora ya kazi na kuimarisha ari ya askari wa Kikosi cha Valantia Zanzibar kupitia **Fungu D06;** Kamati yangu imeridhishwa na juhudi za kuimarisha kikosi kwa kujenga mahanga mapya na nyumba za maafisa kwa kambi mbali mbali za Unguja na Pemba, kikosi pia kinaendelea kuimarisha maendeleo yake kwa kubuni miradi ya maendeleo ambayo itasaidia kukwamua changamoto zao.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati pia, ilibaini kuzorota kwa mradi wa ujenzi wa nyumba za maafisa na hanga la askari katika kambi ya Kikungwi Wilaya ya Kusini ambapo ujenzi wake umedumu kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kwa vifaa kutoka kwa mfanyabiashara aliepewa tenda ya kupeleka vifaa vya ujenzi. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri KVZ kuchukua hatua za haraka kukamilisha ujenzi huu na hatua zaidi za kisheria kuchukuliwa dhidi ya mfanyabiashara huyu.

Kwa upande mwengine, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa wizara kutokana na kuleta mbele ya Baraza hili Tukufu marekebisho ya Sheria ya Kikosi cha Valantia, Namba 5 ya Mwaka 2004 kwa ajili ya kukipa uwezo wa kufanya shughuli za

kiuchumi, biashara na uwelezaji kwa lengo la kutekeleza agizo la Serikali katika kufanya shughuli za uzalishaji mali.

## WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU D 12):

**Mheshimiwa Spika:** Kamati inaipongeza Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa kuweka programu kuu ya **Kusajili vizazi, vifo na Kadi za Utambulisho,** kuwa na malengo ya kuimarisha huduma za usajili kwa ufanisi na kutoa vyeti pamoja na vitambulisho kwa wakati. Kamati inaipongeza Taasisi hii kwa kasi yake ya utoaji wa vyeti kwa njia ya kielektroniki kwa lengo la kuwapunguzia wananchi usumbufu na kuimarisha udhibiti wa taarifa za matukio ya kijamii. Sambamba na hayo, kamati inashauri Serikali kuwapatia fedha za kutosha Wakala wa Usjali wa Matukio ya Kijamii ili kujiendesha bila kuwepo na kiwango kikubwa cha madeni ya ununuzi wa malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa vyeti.

**Mheshimiwa Spika:** Kamati yangu inaomba kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar kuhakikisha wanajisajili kila inapobidi kufanya hivyo, kwani sheria imebainisha matukio yote ambayo yanapaswa kusajiliwa kwa lengo la kuweka wazi taarifa za watu wake ili Serikali iweze kutekeleza vyema mipango yake ya kimaendeleo.

## HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika:** Naomba niwashukuru Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji wao na uzalendo wao na mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu ya Kamati ya Kamati hii. Sambamba na hilo, Kamati yetu inaipongeza sana Serikali kupitia wizara hii kwa uamuzi wake wa kuanza kujenga afisi za Masheha kwa upande wa Unguja na Pemba kwa lengo la kukuza na kuimarisha utawala bora.

**Mheshimiwa Spika:** Mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wairidhie, waichangie na waipitishe Bajeti hii na hatimae waidhinishe makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika:**

***Kwa Niaba ya Kamati yangu;*** **Naomba Kuunga Mkono Hoja.**

……………..…………………….

(Machano Othman Said)

MWENYEKITI,

KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR